

UTAFITI WA AFYA YA UZAZI NA MTOTO NA VIASHIRIA VYA MALARIA WA MWAKA 2022 NCHINI TANZANIA


Vifo Vinavyotokana na Uzazi

Vifo vinavyotokana na uzazi vinajumuisha, vifo vya akina mama wakati wa ujauzito, wakati wa kujifungua na ndani ya siku 42 baada ya kujifungua bila kujumuisha vifo vilivyotokana na ajali au ukatili wa majumbani.

Matokeo ya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2022 nchini Tanzania (TDHS-MIS 2022) yanaonesha kuwa vifo vinavyotokana na uzazi (MMR) kwa Tanzania ni vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 kwa kipindi cha miaka saba kabla ya utafiti. Kiwango cha uhakika wa idadi ya vifo vinavyotokana na uzazi kwa mujibu wa utafiti wa TDHS-MIS 2022 ni kati ya vifo 59 hadi 149 kwa kila vizazi hai 100,000.

Makadirio ya vifo vinavyotokana na uzazi pia yanapatikana kutoka katika Sensa ya Watu na Makazi Tanzania. Taarifa ya idadi ya vifo vinavyotokana na uzazi kutoka katika Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 nchini Tanzania inawiana na taarifa za idadi vifo vinavyotokana na uzazi kutoka katika utafiti wa TDHS-MIS 2022. Aidha, taarifa ya idadi ya vifo vinavyotokana na uzazi kutoka katika Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 nchini Tanzania inaonesha uhakika wa kupungua kwa vifo vinavyotokana na uzazi nchini Tanzania.

Vifo vinavyotokana na Uzazi kwa kila vizazi hai 100,000 katika kipindi cha miaka 7 kabla ya utafiti



Matokeo ya Sensa yanaonesha kuwa idadi ya vifo vinavyotokana na uzazi nchini Tanzania imepungua kutoka vifo 432 kwa kila vizazi hai 100,000 kwa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012 hadi vifo 194 kwa kila vizazi hai 100,000 kwa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022. Aidha, njia ya ukokotoaji wa makadirio ya idadi ya vifo vinavyotokana na uzazi inatofautiana kati ya utafiti wa TDHS-MIS na Sensa. Muda wa rejea katika ukokotoaji wa makadirio ya idadi ya vifo vinavyotokana na uzazi kati ya utafiti wa TDHS-MIS na Sensa vile vile unatofautiana. Makadirio ya ukokotoaji wa idadi ya vifo vinavyotokana na uzazi katika utafiti wa TDHS-MIS 2022 yanajumuisha vifo vilivyotokea katika kipindi cha miaka 7 kabla ya Utafiti, wakati kwa upande wa sensa inajumuisha vifo vilivyotokea katika kipindi cha miezi 12 kabla ya sensa. Kupungua kwa idadi ya vifo vinavyotokana na uzazi kunaonekana katika vyazo hivi vya upatikanaji wa taarifa za vifo vinavyotokana na uzazi. Aidha, kupungua kwa kiasi kikubwa kwa idadi ya vifo vinavyotokana na uzazi kutoka katika vyanzo hivi inatoa uhakika wa kuthibitisha kuwa vifo vinavyotokana na uzazi vimepungua nchini Tanzania.

Je, ni Nini Mwelekeo wa Matokeo Haya?

Kupungua kwa vifo vinavyotokana na uzazi kama ilivyobainishwa na matokeo ya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2022 na Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 inaweza kuwa imechangiwa na utekelezaji wa mambo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa mahudhuri ya kliniki kwa akina mama wakati wa ujauzito, kupungua kwa kiwango cha mimba za utotoni, kuongezeka kwa kiwango cha akina mama wanaojifungua katika vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na kuongezeka kwa kiwango cha akina mama wanaojifungua kwa kusaidiwa na wataalamu wa afya wenye ujuzi. Mafanikio haya yanatokana na uwepo wa sera na mikakati madhubuti inayolenga zaidi makundi ya watu yalio katika hatari ya kukumbwa na vifo vinavyotokana na uzazi. Matokeo haya yanaonesha Tanzania ina mwelekeo mzuri wa kufikia shabaha ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ifikapo Mwaka 2030 ambayo ni kupunguza vifo vinavyotokana na Uzazi hadi kufikia vifo 70 kwa kila vizazi hai 100,000.

Ili kuhakikisha mafanikio haya yanakuwa ni endelevu, jitihada mahsusi zinatakiwa kuwekewa mkazo hususani katika kuimarisha utoaji wa huduma za afya kwa kujenga miundombinu zaidi, kuwekeza zaidi katika vifaa vya uchunguzi wa afya na vifaa tiba, kuongeza idadi ya watumishi wa afya katika vituo vya kutolea huduma za afya vilivyojengwa na serikali katika miaka ya hivi karibuni. Kuimarisha miundombinu ya barabara hususani kwa maeneo ya vijijini, upatikanaji wa uhakika wa nishati ya umeme na maji na huduma nyingine muhimu ili kurahisisha upatikanaji na kuleta huduma ya afya karibu na wananchi.